



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA KIGAMBONI**



[Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa Kigamboni]

Simu: +255 22-2928468
Fax: +255 22-2928469
Baruapepe: info@kigambonimc.go.tz
Tovuti: www.kigamboni.go.tz

S.L.P. 36009,
KIGAMBONI,
DAR ES SALAAM,
TANZANIA.

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na.AB./247/321/01D/152

12 Februari, 2022

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA KUKUSANYA TAARIFA ZA ANWANI
ZA MAKAZI NA POSTIKODI**

Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni anapenda kuwatangazia nafasi za ajira ya muda kwa nafasi za kukusanya taarifa kwenye zoezi la anwani za makazi katika Kata na Mitaa yote ya Manispaa ya Kigamboni.

1. SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Awe na elimu ya kidato cha nne na kuendelea
- ii. Awe raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18-40
- iii. Awe anamiliki simu janja ya android yenye uwezo wa kukaa na chaji kwa muda wa siku nzima
- iv. Awe na barua pepe (email address) inayofanya kazi
- v. Awe ni mkazi wa Kata husika

2. MAJUKUMU

- a) Kugawa/kuandika namba za nyumba, viwanja, na maeneo ya huduma
- b) Kukusanya taarifa za nyumba, viwanja, na maeneo ya huduma za kijamii
- c) Kukusanya taarifa za wamiliki wa nyumba na wapangaji, na kuzituma kwenye mfumo


3. MAOMBI YAAMBATISHWE NA VIELELEZO VIFUATAVYO:

1. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
2. Nakala ya cheti cha kidato cha nne na kuendelea
3. Picha 2 (passport size)

4. JINSI YA KUTUMA MAOMBI

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili ya mwombaji, namba za simu, barua pepe na ziwasilishwe Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni kupitia kwa Mtendaji wa Kata Unapoishi, kabla au ifikapo tarehe 16.02.2022 kwa anwani ifuatayo:

MKURUGENZI WA MANISPAA,
MANISPAA YA KIGAMBONI,
S.L.P 36009,
DAR ES SALAAM.


Erasto N. Kiwale
MKURUGENZI WA MANISPAA
MKURUGENZI WA MANISPAA
KIGAMBONI